



RAISI MHE. SAMIA SULUHU HASSAN

Mbioni Kupunguza Vifo Vya Wajawazito Na Watoto



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na Bi. Senait Fisseha, Mkurugenzi wa Miradi kutoka Taasisi ya Suzan Thompson Buffet

Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan tarehe 31 Mei, 2021 alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Miradi wa Taasisi ya The Susan Thompson Buffet Foundation, Bi. Senait Fisseha, ambayo inajihusisha na masuala ya afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana. Mazungumzo hayo yamehudhuriwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima na Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Aifello Sichwale ambao baadaye walifanya mazungumzo na Bi. Senait Fisseha kwa lengo la kupanga mikakati ya namna taasisi hiyo itakavyofanya kazi na Serikali.

Bi. Senait Fisseha alimueleza Mhe. Raisi Samia kuwa taasisi hiyo ambayo imekuwepo hapa nchini kwa zaidi ya miaka 10 imetumia dola za Marekani takribani Milioni 90 (sawa na shilingi Bilioni 206) kufadhili miradi inayoshughulikia changamoto mbalimbali zinazohusiana na afya ya uzazi kwa wanawake na wasichana. Alibainisha kuwa miradi hiyo imesaidia kukabiliana na vifo vinavyohusiana na ujauzito kwa kuwawezesha wanawake kupanga wakati gani wa kupata ujauzito, wakati gani wa kujifungua, kuepuka ujauzito katika umri mdogo na

kujifungua salama. Bi. Senait Fisseha alishukuru kupata nafasi ya kuzungumza na Mhe. Rais Samia na alibainisha kuwa baada ya mazungumzo hayo taasisi hiyo ipo tayari kuendeleza miradi hiyo kwa kushirikiana na Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Kwa upande wake, Mhe. Raisi Samia aliishukuru taasisi hiyo kwa mchango wake katika masuala ya afya ya wanawake hapa nchini na alimhakikishia kuwa Serikali ya Tanzania ipo tayari kushirikiana naye ili kukabiliana na changamoto zinawakabili wanawake na wasichana katika masuala ya afya hususan afya ya uzazi.

MAPENDEKEZO:

1. Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) tunapenda kumpongeza Raisi pamoja na viongozi wenzake kwa juhudi za kuhakikisha kuna makubaliano na mikakati mbalimbali baina ya Tanzania, Wadau wa Maendeleo na taasisi binafsi kuhakikisha afya ya mama na mtoto inaboreshwa na vifo vya wajawazito na watoto vinapungua nchini.

2. Tunatoa rai kwa Serikali kuimarisha mazingira wezeshi kwa wajawazito ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kipindi cha ujauzito, wakati wa kujifungua na mara baada ya kujifungua; ikiwemo kuwekwa mpango mkakati mahsusi kwa ajili ya kumhakikishia Mwanamke huyu uzazi mwema na siyo wa kumhatarishia maisha yake. Ikumbukwe kuwa ili taifa liendeleo linahitaji nguvu kazi na wanawake ndio waliobeba jukumu hili zito la kuleta nguvu kazi duniani.

3. Pia, tunatoa hamasa kwa Serikali na wadau wengine wa maendeleo kuongeza uwekezaji zaidi wa bajeti katika sekta hii ya afya. Kuna umuhimu mkubwa wa kuwekeza zaidi kwa wataalam wa afya wakiwemo wakunga hospitalini ambao wamekuwa changamoto wakati wa kutoa huduma kwa kina mama wajawazito. Wanawake wamekuwa wakikutana na adha za huduma hafifu wakati wa kujifungua na wakati mwingine lugha zisizo na staha zinazofanya wengine wakate tamaa kutumia huduma za afya hospitalini. Hali hii wakati mwingine inasababisha na kulazimisha wanawake hususan wa vijijini kulazimika kujifungulia nyumbani ambapo wanahatarisha maisha yao na watoto walioko tumboni.

TGNP pamoja na wana AZAKI wengine tutaendelea kumuunga mkono Raisi kwa kujenga nguvu za pamoja katika kampeni yake ya kukomboa maisha ya mama na mtoto Tanzania.

“Inawezekana Vifo vya Wanawake na Wasichana Vinavyotokana na Uzazi kuwa Historia: Twende Pamoja Asiachwe Mtu Nyuma.”